

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU, 2019

KISWAHILI KIDATO CHA 2

LUGHA

JINA _____

_____ NAMbarI _____ DARASA _____

1. UFAHAMU (Alama10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekeea kushuhudiwa kwamsururu wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiaashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti.

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kipingwa. La kufahamishiwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimaghari wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji. Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipyä ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wakuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

Maswali

a) Yape makala haya anwani mwafaka.

(alama 1)

Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu.

(alama 2)

“Ugatuza nchini Kenya ni mfumo wa kibepari” Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala.

(alama 1)

b) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuza

(alama 2)

Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuza umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu

(alama 2)

Eleza maana ya neno lifuatalo

(alama 2)

Ugatuza

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama30)

- a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

/a/

/u/

- b) i) Ngeli ni nini? (alama 1)

- ii) Maneno haya yamo katika ngeli gani? (alama 2)

Tunda

Kipepeo

- c) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo (alama 3)

Sikumkaribisha

d) Andika kwa wastani (alama 2)

Magoma hayo yatachezwa mawanjani

e) Tofautisha sentensi zifuatazo. (alama 2)

- i) Baniani mwenyewe ni huyu.
- ii) Baniani mwenye mali amelegeja.

f) Tunga sentensi ukitumia VIELEZI vya;na upigie mstari (alama 3)

a) wakati

b) mahali

c) namna

g) Tunga sentensi kuonyesha maana mbili za neno

chuma (alama 2)

4. ISIMU JAMII (Alama 5)

i) Eleza maana ya **Isimu Jamii** (alama 1)

ii) Eleza sifa nne za mazungumzo kati ya daktari na mgonjwa. (alama 4)

5

FASIHI SIMULIZI

(i) Eleza sifa sita za fasihi simulizi.

(ii) Ushairi ni kwa malenga.Taja watendaji wa tanzu hizi.

Nyimbo _____

Hadithi _____

(iii) Tofautisha kati ya:

Hurafa na Hekaya
